# UTANGULIZI

Masikitiko makubwa ambayo mtu atakuwa nayo pale atakapokuwa amebakiwa na sekunde chache afe, si fedha anazoziacha benki, wala familia anayoiacha au marafiki anaowaacha. Bali masikitiko makubwa yatakuwa ni uwezo mkubwa uliolala ndani yake na anakufa bila kuutumia.

Muda huo anaweza akatamani uwezo huo ungekuwa kama fedha amgawie nduguye au rafikiye, lakini haitawezekana kwani uwezo alionao mtu ni mali yake mwenyewe na hawezi kumhamishia mtu mwingine. Ndipo mtu anapotamani aongezewe muda wa kuishi hata kwa siku moja lakini hilo halitawezekana kwa sababu ya ukomo wa muda aliopewe binadamu.

Tofauti na wanyama wengine binadamu tumeumbwa kwa namna ya tofauti. Wanyama wamepewa uwezo wa kuwafanya wazaliane, wale, wajilinde na maadui na mwisho wafe. Binadamu tumeumbiwa uwezo mkubwa zaidi ya huo, yaani uwezo wa kutenda mambo makubwa na ya kushangaza zaidi ya kula, kujilinda na kuvaa. Hivyo njia pekee ambayo mtu anaweza kujitofautisha na wanyama ni kutumia uwezo wake kufanya mambo tofauti au zaidi ya wanyama. Wanyama wengi wamefanana kwa sura na kwa matendo yao lakini binadamu tumefanana kwa sura lakini kila mtu ana uwezo ndani yake ambao akiuamsha anaweza kufanya mambo makubwa na tofauti kabisa na watu wengine.

Mambo makubwa ambayo yametendeka duniani na kwa ufahamu wako unayaona ni makubwa na miujiza ni kwa sababu ya watu waliojaribu kutumia hazina kubwa sana waliyokuwa nayo, japo kwa kiasi kidogo.

Kila mtu ana uwezo mkubwa na wa kipekee ndani yake. Uwezo huo ni kwa ajili ya kutimiza kusudi la kuwepo kwake hapa duniani. Na kusudi hilo litatimia pale tu mtu atakapothubutu kutumia uwezo huo. Hiki ni kitu pekee ambacho mtu anaweza kujivunia nacho, kwani kuitumia hazina hii mtu anaweza kupata mafanikio yoyote yale na kwa kiwango chochote kile. Uwezo huu ni hazina kubwa sana inayompa mtu thamani kubwa sana hapa duniani. Mafanikio yoyote makubwa anayoweza kuyapata mtu yanategemea sana matumizi ya hazina hii kubwa ambayo anaipata tangu kuzaliwa kwake.

Aliyekuwa mwandishi na mnenaji mashuhuri Dr Myles Munroe alisema; ***"The wealthiest place in the world is not the gold mines of South America or the oil fields of Iraq or Iran. They are not the diamond mines of South Africa or the banks of the world. The wealthiest place on the planet is just down the road. It is the cemetery."***Akinamaanisha kuwa sehemu tajiri zaidi duniani sio migodi ya dhahabu iliyopo Amerika ya Kusini, au ardhi yenye mafuta iliyopo Irak na Iran. Sio migodi ya almasi zilizopo Afrika Kusini au wala siyo benki za dunia. Sehemu tajiri katika dunia ipo karibu yako. Ni makaburini. Unaweza ukashangazwa na kauli hii kwani umezoea kuwa mtu aliyekufa, habari yake inakuwa imeisha kwani huzikwa yeye kama yeye au wachache huwazika na baadhi ya mali. Sasa kwa nini Dr Myles alisema utajiri mkubwa upo makaburini? Je watu huwa wanakufa wakiwa wamemeza fedha, almasi, dhahabu, au shaba? Inashangaza ehe!

Jibu ni hapana si kwamba watu wanazikwa na mali walizovuna kipindi cha uhai wao, la hasha, bali watu wengi wamezikwa na uwezo mkubwa ambao wangeutumia kabla hawajafa wangeweza kutengeneza utajiri mkubwa sana. Mtu huzaliwa na uwezo mkubwa ndani yake

na hakuna mtu mwingine anayeweza kuutumia uwezo huo isipokuwa yeye mwenyewe. Hivyo ikitokea amekufa bila kuutumia uwezo huo, huzikwa nao.

Matokeo makubwa tunayoyaona duniani ni kwa sababu binadamu alijaribu kutumia angalau kiasi kidogo tu cha uwezo wake. Licha ya kujaribu kutumia kiasi kidogo tu cha uwezo huo, dunia imejaa maajabu ambayo macho yetu, masikio yetu na fikira zetu zinashangaa kwamba ni kwa namna gani binadamu ameweza kuyafanya hayo yote. Ona miundombinu kama barabara na majengo makubwa na ya kushangaza yaliyopo duniani. Magari makubwa na ya thamani kubwa na teknolojia ya mawasiliano ambazo kila siku zainazidi kushangaza. Haya yote ni matumizi kidogo tu ya uwezo ambao binadamu anao. Tafiti zinaonesha kuwa hata haya unayoyashangaa, wahusika wametumia si zaidi ya 15% ya uwezo wao. Kulingana na uhalisia huo wewe umetumia kiasi gani cha uwezo wako?

Kama makaburi yamebeba watu ambao walitumia kiasi kidogo sana cha uwezo wao, basi kiasi kikubwa ambacho bado kimelala kingeleta mapinduzi makubwa sana duniani, na kuifanya dunia kuwa sehemu nzuri zaidi ya kuishi. Watu wamekufa na vumbuzi kubwa ambazo zingeboresha sana maisha ya watu wengine. Wengine wanakufa na vipaji vikubwa ambavyo vingeburudisha na kuhamasisha sana wengine. Kuna ambao pia wamekufa na vitabu ambavyo kama vingeandikwa vingefundisha au hata kuburudisha na kuhamasisha watu kuboresha maisha yao. Wengine wamekufa na majengo makubwa akilini mwao ambayo wangeyajenga yangeleta utajiri mkubwa sana duniani. Ningeweza kuendelea kukupa mifano mingi ya nini makaburi yamebeba. Lakini itoshe kuona kuwa dunia inapata hasara kubwa sana pale mtu anapokufa bila kutumia uwezo wake mkubwa alio nao ndani yake.

Kwa sababu uwezo wenyewe hatuuoni kwa macho isipokuwa kwa matokeo yake, si rahisi kuona thamani ya uwezo ambayo wewe au mtu mwingine ameibeba. Kama tungelinganisha uwezo wa binadamu na mnyama, tungeweza kusema kila mtu ana tembo mkubwa aliyelala ndani yake ambapo binadmau wengi wanakufa wakiwa wamekula mkia wake tu.

Uwezo ni nguvu ambayo unaweza kuitumia kufanya makubwa. Nguvu hizo hazihusishi yale uliyokwisha kuyafanya bali yale unayotarajiwa kuyafanya au yale mtu aliyekufa alitarajiwa kuyafanya. Hivyo kama bado upo hai jua kuna tembo mkubwa ambaye amelala tu ndani yako anasubiriwa kuliwa.

Kuna watu takribani milioni nane duniani sasa, lakini hakuna mtu anayefanana na wewe. Kila mtu ameumbwa kwa namna ya kipekee sana ili kutimiza kusudi maalumu. Kusudi hilo linatimia na kuleta matokeo makubwa yenye kuinufanisha dunia pale mtu anapotumia uwezo wake vizuri. Ulipokuwa unaumbwa tayari ulishawekewa uwezo huo mkubwa ndani yako. Mafanikio yako yanategemea umetumia kiasi gani mpaka sasa. Lakini kama unaona hujafanya maajabu yoyote mapaka sasa haimanishi kuwa huna nyenzo ya kufanya makubwa ambayo watu wengine wameyafanya bali uwezo huo unao lakini haujautumia.

Matatizo ambayo watu wengi wanahangaika nayo kama vile ya kiuchumi, mahusiano, binafsi na afya ni matokeo ya kutoutumia uwezo wao ambao tayari wanao ndani yao. Kuna watu wengi wamekuwa wakihangaika na matatizo ya kipato kidogo kwa muda mrefu bila ya kujikwamua. Pia wengine wamekuwa wanaishi maisha ambayo hawayapendi lakini wameshindwa kutoka katika zizi hilo. Watu hao wamekuwa wakiwaonea wivu watu wengine ambao wanaonekana wamefanikiwa wakiamini kuwa hao wamependelewa au wana bahati. Lakini matatizo haya na mengine mengine mengi ni kwa sababu ya kutoweza kutumia hazina kubwa ya uwezo uliopo ndani yao.

Sababu mojawapo ya kutotumia uwezo huo ni kutojua kuwa kuna hazina kubwa yenye thamani kubwa ndani ya kila mtu. Hivyo watu wameendelea kuishi na matatizo licha ya sululisho lililopo ndani yao. Wapo wengine wanaojua kuwa wana uwezo mkubwa ndani yao lakini wameshindwa kuuamsha uwezo huo na kufanya makubwa au hata pale walipojaribu kuutumia walifanikiwa kutumia kwa kiasi kidogo sana. Hii ni sababu nyingine ambayo inawafanya watu kuendelea kuishi maisha ya kawaida ingali wangeweza kupata mafanikio makubwa zaidi ya kuishangaza dunia. Sababu nyingine ni jamii inayotuzunguka inayolazimisha watu kufanana ambayo imekuwa ni sumu ya kuufanya uwezo wako kuendelea kulala.

Ndugu yangu naamini kuna mafanikio uliyokwisha yapata, uwe unayaona makubwa au madogo, lakini napenda kukuambia kuwa ulichokipata ni kama tone tu la maji kwenye bahari, yaani ni kiasi kidogo sana ukilinganisha na ulichostahili. Kama bado upo hai una nafasi ya kufanya makubwa zaidi ya sasa, yaani ambayo yataonekana kama miujiza mbele yako na dunia. Jambo hili ndilo lililonisukuma kuandika kitabu hiki, ili uweze kuishi maisha unayostahili kwani ulistahili ngazi za juu zaidi ukilinganisha na ulipo sana. Haya yote yatawezekana kwa kuamsha uwezo wako halisi.

Kupitia kitabu hiki utaenda kujua kiundani maana halisi ya uwezo halisi ambayo ni hazina uliyoibeba mpaka sasa. Pia utaenda kujua namna ya kuamsha uwezo wako na kuanza kuutumia ili kupata mafanikio makubwa. Kitabu hiki kimependekeza hatua mahususi za kuchukua mara moja ili kuamsha uwezo wako na kuanza kuona ukuaji wa kuelekea kwenye mafanikio makubwa unayostahili. Nikupongeze kwa hatua uliyochukua ya kukipata kitabu hiki na karibu uendelee kukisoma na kunufaika. Naamini hutajutia uamuzi wako wa kununua na kukisoma kitabu hiki na ni maombi yangu kwako ufanikiwe kupitia usomaji huu.

Alfred Mwanyika.